



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO

Unapojibutafadhalitaja:

Kumb.Na.CDC/08/2/VOL.III/198

Tarehe: 01/12/2020

Kamishna wa Ardhi Msaidizi (M),
S.L.P 484,
GEITA.

Yah: OMBI LA KAMPUNI YA SUPREME PERCH LTD KUPATIWA NA KUMILIKISHWA KIWANJA NA.7 KITAL 'G' RUBAMBANGWE .

Husika na mada tajwa hapo juu,pia rejea barua yangu yenye kumb.Na. CDC/08/2/VOL.III/158 tarehe 9/09/2019 ambayo imeambatanishwa kwenye barua hii.

2. Nakutumia taarifa muhimu za Kampuni husika pamoja na taarifa za ardhi inayoombwa kumilikishwa.
3. Hivyo naomba kuwasilisha kwako mambo yafuatayo ambayo yanatakiwa na ofisi yako kama ifuatavyo:
 - Andiko la mradi wa kiwanda cha kuchakata minofu ya samaki unaotarajiwa kutekelezwa.Andiko hilo limeonesha mambo mbalimbali yakiwemo mpango wa uendelezaji mradi , muda wa mradi , teknolojia itakayotumika na mtaji wa Kampuni.Vilevile manufaa ya Mradi huo kwa jamii inayozunguka yameeelezwa
 - Nakala ya taarifa ya Kampuni kutoka Mamlaka ya usajili wa Makampuni (BRELA)

- Taarifa ya hali halisi ya uwandani hadi kufikia sasa ni kwamba eneo hilo tayari lilishalipwa fidia kwa mwenyeji mmoja aliyekuwa anamiliki kimila na vilevile ardhi hiyo tayari imeshapimwa na kupewa namba ya kiwanja Na.7 Kitalu 'G' Rubambangwe. Vilevile ardhi hiyo kwa sasa bado ipo wazi ikiwa na miti iliyopandwa na mmiliki wa awali kabla ya kutwaliwa. Nyuma ya barua hii nimeambatanisha picha zinazoonesha hali halisi hiyo

4. Kwa maelezo hayo naiomba Ofisi yako iendelee na taratibu za kisheria za umilikishaji wa kiwanja hicho.

Nawasilisha kwa hatua stahiki,



Tiberius G. Rweyemamu

Kny: Mkurugenzi Mtendaji (W)

CHATO.

Nakala:

Mkurugenzi Mtendaji (W) -aione kenye jalada

CHATO.